JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA KUMI NA MBILI

21 JUNI 2010

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA KUMI NA MBILI – TAREHE 21 JUNI, 2010

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha

2009/2010 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA MAKAMU WA RAIS:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

77. **MHESHIMIWA AZIZA SLEYUM ALLY (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kwenye nchi yetu kuna maeneo mengi ya vijijini na mijini ambayo hayajapatiwa umeme vikiwemo Vituo vya Afya ambavyo kutokana na hali hiyo vinatumia koroboi:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kupeleka angalau umeme wa *solar* katika Vituo vya Afya na Zahanati mbalimbali kama vile Puge – Bukene, Itobo na kwingineko nchini.

78. MHESHIMIWA CLEMENCE BEATUS LYAMBA (MIKUMI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kituo cha Afya cha Kidodi katika Tarafa ya Mikumi yenye wakazi wapatao 72,250 na Hospitali ya St. Francis vinahudumia wakazi zaidi ya 100,000 hazina jokofu hata moja la kuhifadhia maiti:-

Je, Serikali itasaidiaje kupatikana kwa jokofu angalau moja katika Kituo cha Afya cha Idodi na moja Hospitali ya St. Francis kwa ajili ya kuhifadhia maiti katika maeneo hayo.

WIZARA YA MIUNDOMBINU:

79. MHESHIMIWA HASNAIN GULAMABBAS DEWJI (KILWA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu: Wananchi wa Kiranjeranje kwenye Wilaya ya Kilwa hawajalipwa fidia za nyumba zao katika barabara kuu ya Nangurukuru – Mbwemkuru na Wilaya ya Kilwa tayari imefanya tathmini ya gharama zipaswazo, lakini miaka mitatu imeshapita bila fidia hizo kulipwa:-

Je, lini wananchi hao watalipwa haki zao.

80. MHESHIMIWA MGENI JADI KADIKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu:- Ajali nyingi zinapotokea majini huwa ni vigumu kupata idadi ya watu wanaopoteza maisha kwa kuwa vyombo hivyo hujaza watu wengi na mizigo kinyume na sheria:-

Je, Serikali inawachukulia hatua gani wamiliki wa vyombo hivyo wanaokiuka sheria, pamoja na wadhibiti wa vyombo hivyo **(SUMATRA).**

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

81. MHESHIMIWA MICHAEL LEKULE LAIZER (LONGIDO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Mradi wa maji wa **ADB** Wilayani Longido umejengwa chini ya viwango na usimamizi hafifu unaofanywa na Mhandisi wa Wilaya ya Monduli ambaye hana nafasi kubwa ya kutembelea Longido:-

Je, ni lini mradi huo utakabidhiwa kwa Mhandisi wa Wilaya ya Longido.

82. MHESHIMIWA SIJAPATA FADHILI NKAYAMBA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Wananchi wa kijiji cha Mlela Wilaya ya Kigoma Vijijini wana matatizo ya maji ambapo hutumia maji kutoka katika visima walivyochimba wenyewe ingawa chanzo cha maji kilichoko kijijini kwao maji yake yanapelekwa kwa wananchi wa kijiji jirani cha Kidahwe:-

(a) Je, kwa nini Serikali isiwachimbie visima virefu na vifupi wananchi hao kwa sababu chanzo chao cha maji kilipelekwa Kidahwe;

(b) Je, ikiwa chanzo hicho cha maji kinajitosheleza kwa nini wananchi wa Mlela nao wasitumie maji hayo.

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

83. MHESHIMIWA CASTOR RAPHAEL LIGALLAMA (KILOMBERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi:- Katika Wilaya ya Kilombero kuna kituo (Lumemo Resourses Centre) kinachotoa elimu kwa walemavu chini ya mpango wa "*Itinerant Teaching Programme Access and Education Quality Improvement*":-

(a) Je, Serikali inautambua mpango huo;

(b) Kama unatambulika, Je; ni lini walimu hao watapewa pikipiki mpya ili waweze kutoa

huduma kikamilifu hasa ukizingatia kuwa pikipiki walizonazo ni chakavu na hazifai kuwa barabarani.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

84. MHESHIMIWA AHMED MABKHUT SHABIBY (GAIRO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Jimbo la Gairo lina vijiji vingi na vikubwa vyenye idadi kubwa ya watu na hivyo kustahili kupatiwa huduma ya umeme ambao unapita katika maeneo hayo tokea Mkoa wa Dodoma, ambako unasambazwa kwenye vijiji vyenye idadi ndogo ya watu:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba huduma hiyo ya umeme kwa Kanda ya Kati inasambazwa kwa kufuata matakwa

ya watu binafsi na si kwa umuhimu na wingi wa watu;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika Kata za Chakwale, Kibedya na Rubeko ambazo zipo umbali wa kilomita 10 toka umeme ulipo na Mheshimiwa Rais aliahidi kuwa zitapatiwa umeme.

85. MHESHIMIWA VICTOR KILASILE MWAMBALASWA (LUPA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Serikali kupitia bajeti yake ya Mwaka 2009/2010 imetenga fedha kupitia Wakala wa Umeme Vijijini **(REA)** kwa ajili ya kupeleka umeme katika vijiji vya Lupa, Sangambi na Mlimanjiwa Wilayani Chunya, na tayari Mkandarasi wa kujitegemea wa kufanya kazi hiyo tayari amepatikana:-

Je, ni Kampuni gani imepewa zabuni hiyo na kazi itaanza lini.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

DODOMA **DKT. T.D. KASHILILAH**
21 JUNI, 2010 **KATIBU WA BUNGE**

SAHIHISHO KWENYE HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA KUMI NA MBILI - TAREHE 21 JUNI, 2010

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:

Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

DODOMA **DKT. T.D. KASHILILAH**
21 JUNI, 2010 **KATIBU WA BUNGE**